# Uwekaji wa Malengo ya Kielimu

Mtoto wako ana sifa za kuwekwa kwenye Mpango wa Elimu Inayomlenga (IEP), hatua inayofuata ni gani? Utakutana na timu yako ya IEP kuweka malengo kwa ajili ya mtoto wako. Timu ya IEP inajumuisha wataalamu wa elimu, wafanyikazi wa shule, wazazi, wanafunzi (wa miaka 14 au zaidi), na wengine wenye ufahamu maalumu wa mtoto wako.

## Lengo ni Nini?

Lengo la kupimika la kila mwaka ni kauli juu ya kile kitu ya IEP inakubaliana kwamba kinafaa kwa mtoto kujaribu kukikamilisha wakati wa mwaka wa masomo katika eneo mtoto ana mahitaji. Malengo yanaweza kuandikwa ili kupima maendeleo kimasomo na kiutendaji wa majukumu. Kwa kuwa lengo limeandikwa kwa ajili ya mahitaji maalumu ya mtoto wako, timu ina nafasi ya kuamua yatakuwa malengo gani. Wewe, kama mzazi, una jukumu muhimu katika kuunda malengo haya.

### *Hatua za Uwekaji Malengo*



**Maudhui:** Lengo la kupimika la kila mwaka lina:

1. Kiwango cha Sasa cha Mafanikio na  Utendaji wa Kimajukumu (PLAAFT), na
2. Lengo la mwaka.

Kiwango cha sasa cha utendaji wa mwanafunzi wako ni muhimu katika kuhakikisha malengo haya yanalenga mahitaji ya kielimu na kiutendaji ya mwanafunzi wako. Kwa wanafunzi ambao wanafanyiwa tathmini mbadala, lengo lazima pia lijumuishe vigezo au malengo ya muda mfupi (STOs), ambayo ni hatua ndogo-ndogo za kumsaidia mwanafunzi kufikia lengo kuu. Maelezo yafuatayo yanaonyesha hatua katika uwekaji lengo.

### *Mafanikio ya Kielimu na Utendaji wa Kimajukumu (PLAAFP) wa Sasa*

Mafanikio ya kielimu na utendaji wa kimajukumu (PLAAFP) wa sasa vimekitwa katika takwimu za tathmini na vinafaa kuwa maalumu kwa jinsi ulemavu wa mwanafunzi unaathiri maendeleo yake ya kielimu na kiutendaji. PLAAFP inafaa kujibu mwaswali haya:

- Mtoto anaweza kufanya nini?
- Ni jinsi gani ulemavu wa mtoto unaathiri kushiriki na maendeleo yake katika mtaala wa jumla

(mtaala mkuu) (au shughuli zinazofaa kwa watoto wa umri wa chekechea)?

Ili PLAAFP iwe kama mahali pa kuanzia, lazima ipimike, ili maendeleo ya mwanafunzi yaweze kupimika.

### *Malengo ya Muda Mfupi (STO) au Vigezo*

Malengo ya muda mfupi (STO) au vigezo huhitajika tu kwa wanafunzi wanafanyiwa tathmini mbadala. Hata hivyo, yanaweza kutumiwa, kama timu itaona kwamba yatamfaidi mwanafunzi. Haya malengo ya muda mfupi hugawanya stadi maalumu katika vijisehemu vya hatua ili kufikia lengo la mwaka.

Malengo ya muda mfupi na vigezo ni muhimu kwa sababu:

- Yanaelezea kile mwanafunzi anatarajiwa kukisoma katika eneo fulani katika kipindi maalumu.
- Yanaamua kiwango cha maendeleo mwanafunzi anapata kuelekea kufikia kwenye lengo.

## Ni nini IEP ya mtoto wako inapaswa kuwa nacho?

- **Malengo ya Kupimika ya Kila Mwaka**

Malengo ya kupimika ya kila mwaka huelezea stadi au mafunzo timu ya IEP ingependa mwanafunzi kusoma au kuimarika. Malengo haya lazima yawe ya kupimika na yaelezee kile mwanafunzi atatarajiwa kusoma katika kipindi cha miezi 12.

- **Malengo ya Kupimika ya Baada ya Sekondari**

IEP za mpito pia zinahitajika kuwa na malengo ya kupimika ya baada ya sekondari. Kwa kawaida huwa yameandikwa kwa maneno ya mwanafunzi mwenyewe.

- **Malengo ya Mwanafunzi**

Kuandika malengo ya kupimika ya kila mwaka (na malengo ya muda mfupi au vigezo vya mwanafunzi anayefanya tathmini mbadala) ni sehemu kuu ya mchakato wa IEP. Malengo ya kila mwaka yanaangazia kufikia mahitaji ya mtoto ambaye anahitaji elimu maalumu na huduma zinazohusiana. Malengo yanaelekezwa kwa:

1. Kuzibwa mwanya baina ya uwezo wa mwanafunzi ulioelezwa na hali ya sasa ya mafanikio ya kielimu na utendakazi wa kimajukumu.
2. Kumsaidia mtoto kuongezeka kiuwezo.

Malengo ya kila mwaka (na malengo ya muda mfupi au vigezo) huwakilisha jinsi nguvu zitaelekezwa ili kusuluhisha mahitaji ya mwanafunzi ilivyoorodheshwa katika IEP. Yanalenga katika kupunguza matatizo ambayo yanayotokana na ulemavu wa mwanafunzi kuingilia masomo au utendaji wake kielimu.

## Aina za Malengo ya Kielimu

Mengi ya malengo ya kielimu huwa katika moja au zaidi ya maeneo haya:

- Masomo ya darasani – kusoma, kuandika lugha, tahajia, hisabati, sayansi
- Kujitegemea – kula, kuvaa, kununua, kusafiri, usalama, kupanga bajeti
- Stadi za Kimwili – kuendesha baiskeli, kuruka, kuandika, kufunga vifungo kufunga zipu
- Stadi za Kijamii/Hisia – kushiriki, kufanya urafiki, kujaribu mambo mapya, kutabasamu, kuitikia utani
- Stadi za Kiufundi/Kabla-ya ufundi – kufuata maelekezo, kukamilisha kazi, kutumia vifaa, kufanya mabadiliko, stadi za kijamii zinazofaa katika mazingira ya kazi
- Mazoea ya – kukabiliana na uchokozi, kushinda katika jukumu, kufuata maagizo, mwenendo unaofaa darasani, kukabiliana na mihemko kwa njia nzuri
- Uzungumzaji/Mawasiliano – kujifunza lugha ya ishara, utamkaji, na kumbukizi ya matamshi.

Takwimu za tathmini hutumika kujua maeneo ya mahitaji. Malengo na huduma faavu za IEP zinafaa kuelekeza katika uwekwaji mahali panapofaa. Baada ya kuandika malengo na kuamua ni huduma gani zinahitajika, timu hii inafaa kuuliza, ‘'Ni wapi mwanafunzi anaweza kupokea huduma hizi katika mazingira yasiyokuwa ya kubana?’

## Elimu ya Jumla na IEP

Hitaji la mbinu-saidizi na kubadilishwa muundo katika programu ya elimu ya jumla linafaa kushughulikiwa katika mchakato wa uwekaji malengo ya elimu na yanaweza **kujumuishwa katika IEP**. Mbinu-saidizi na kubadilishwa muundo kunalenga mafunzo katika mtaala wa jumla na pia katika tathmini ya jimbo na ya wilaya. **Ili mwanafunzi atumie mbinu-saidizi katika tathmini ya jimbo na wilaya, matumizi ya mbinu-saidizi lazima yawe yameandikwa katika IEP na vitumiwe darasani kila wakati.**

**Mbinu-saidizi** ni mabadiliko ya jinsi—njia mambo hufanyika kwa kawaida katika shule/darasa/tathmini, ili kumpa mwanafunzi fursa sawa kushiriki. Mabadiliko hayo huwa hayatofautiani kimsingi au kwa kiasi kikubwa au kupunguza viwango vya shule, wilaya au jimbo. Mwanafunzi anasoma vitu sawa (mtaala wa jumla) kama wanafunzi wengine.

**Mifano ya Mbinu-Saidizi**

- Gawa kazi za wanafunzi katika vipande vifupi vifupi. Toa vikumbusho vya mara kwa mara.
- Ongeza muda wa kukamilisha kazi za mwanafunzi.
- Toa mjarabu kwa mazungumzo. Ongeza muda wa kukamilisha mjarabu.
- Mpe mwanafunzi nakala ya matini ya darasani. Tumia michoro ya kupangilia uandishi wa matini.

- Kalisha mwanfunzi pahali pasipokuwa na usumbufu. Tumia mikrofoni na vipaaza sauti darasani.
- Toa matini kwa muundo mwingine kama vile Braille au sauti.

**Mageuzi**

Mageuzi hubadilisha msingi au kiasi kikubwa au kupunguza viwango au vigezo. Hubadilisha kile mtoto anasoma. Mageuzi yanaweza kuwa mabadiliko ya muundo wa programu, maudhui au mafundisho.

**Mifano ya Mageuzi**

- Kupunguza au kurahisisha nyenzo, kazi za mwanafunzi, kazi ya nyumbani, miradi ya shule au mijarabu.
- Gredi kwa vigezo vya Pass/Fail kama gredi zimeanguka chini ya gredi ya “C”. Gredi kazi iliyorekebishwa na mwanafunzi.
- Hakuna kutoa kazi ya nyumbani au kupunguza kazi ya nyumbani kwa somo.
- Badilisha matarajio ya mafundisho ya darasani kwa mwanafunzi (mwenye ulemavu na Mpsngo wa Kubadili Mafunzo)

## Je, Mtoto Wangu Anafaa Kuwa na Malengo Mangapi?

Kama IEP ina malengo mengi, inaweza kuchanganya au kukatisha tamaa kila mtu. Ni muhimu kuwa na matarajio ya kiuhalisia juu ya idadi ya vitu mwanafunzi anaweza kufanya. Jaribu kuweka idadi ya malengo iwe ya kuwezekana. Kwa kawaida inatosha kuweka lengo moja kwa kila eneo kubwa la shaka. Kwa mfano, unaweza kuwa na lengo kwa kusakata hesabu, kusoma hadithi, stadi msingi za kusoma, mafundisho, na mazoezi ya viungo yaani PE.

Shule inahitajika kutumia tathmini ya kupima maendeleo katika mtaala mkuu, au ule mtaala unaohitajika na jimbo kwa wanafunzi wote. IDEA pia inasisitiza kwamba watoto wenye ulemavu wanafaa kufikia mtaala wa jumla. Mara nyingi, inawezekana kuchagua malengo katika maeneo ya mtaala mkuu (mtaala wa jumla) ambao watoto watakuwa wanasoma. Hata kama mtoto wako hataweza kutenda katika kiwango cha wanafunzi wa kawaida, wewe kama mzazi unaweza kupenda kuhimiza upangaji wa malengo ya mtoto wako na mtaala mkuu. Hili litasaidia mtoto wako kufikia mtaala mkuu, na apige hatua pole pole kwayo. Ingawa, kipaumbele kinafaa kuwa katika mambo ambayo mtoto wako anahitaji zaidi.

## Je, Jukumu Lako ni Gani Katika IEP ya Mtoto Wako?

Wazazi hutekeleza jukumu muhimu katika mchakato. Unamfahamu mtoto wako vyema zaidi na picha ya uwezo na udhaifu wa mtoto wako vitakuwa muhimu kwa timu katika kuunda na kuandika

malengo ya mtoto wako. Labda ni muhimu ujiulize maswali yafuatayo unapoendelea kujiandaa kusaidia timu yako katika kuandika malengo ya mtoto wako:

- Je, ni kitu gani mtoto wangu anaweza au asichoweza kufanya kwa sasa? Je, ni kipi kiwango chake cha sasa ujuzi na ufahamu? (Haya yatatajwa katika PLAAFP.)
- Je, ni jinsi gani hitaji hili la mtoto wangu linahusiana na ulemavu wake?
- Je, ni kitu gani ningependa mtoto wangu akijue au aweze kukifanya kufikia mwisho wa mwaka huu?

Je, hili ni tarajio linalowezekana?

- Je, kwa nini mtoto wangu asiweze kufanya sasa? Ni kipi katika ulemavu kinachohitilafiana na kufikia

lengo? Ni nini kinafaa kushughulikiwa?

- Je, ni wapi mahali pa kuanzia kwa mtoto wangu?
- Je, lengo ni kitu kinachoweza kupimika? Je, ni lini tutajua kwamba lengo

limekamilika? Je, tunalotafuta linaweza kuonekana na kupimika?

- Je, tunahitaji hatua za kati kama vila malengo ya muda mfupi au vigezo ili kufikia hilo lengo? (Kwa wanafunzi wanafanyiwa tathmini mbadala, haya yanahitajika.)
- Kama tunatumia malengo ya muda mfupi au vigezo, ni jinsi gani tutavipima? Je, kuna hatua, za wazi zinazoonekana ambazo zitamkuza mwanafunzi kutoka PLAAFP hadi kwenye malengo ya mwaka ya kupimika?
- Wafanyikazi wa shule wanafaa kujua kuandika malengo faavu ya mwaka yanayoweza kupimika. Si lazima liwe jukumu la wazazi. Ingawa, kuwa na uelewa mzuri wa jinsi mchakato unavyokwenda na sifa za malengo mazuri kunaweza kusaidia wazazi kuwa na washirika wenye ufahamu katika mchakato na kufuatilia maendeleo ya mwanafunzi. Wazazi wana kila haki ya kutarajia malengo kwa mtoto wao yalingane na mahitaji ya mtoto na yasakatwe ili yasaidie kufaulu kwa kwa mtoto.